

Kujifunza kufanya kazi na herufi na nambari

Rasilimali za familia



Mfumo wa Kujifunza Miaka ya Mapema (Early Years Learning Framework) ni mfumo wa kitaifa wa kujifunza unaotumika katika shule za mapema na huduma zote za utotoni. Inaongoza ufundishaji na kujifunza na matokeo matano ya kujifunza ambayo husaidia watoto kuwa wanafunzi hodari na wenye uwezo.

Matokeo ya kujifunza 5 ni juu ya watoto kuwa wasemaji wenye ufanisi. Hii inamaanisha wanaweza kujifunza juu ya lugha, kusikiliza na kujibu sauti na mifumo katika kusema, hadithi na nyimbo. Watoto wanaweza kutumia teknolojia katika maisha yao ya kila siku kuchunguza habari mpya na kuwakilisha maoni yao. Wanajifunza juu ya dhana za hesabu kama nambari, kuhesabu, kipimo na umbo.

Kwa habari zaidi juu ya Early Years Learning Framework nenda kwa:
<https://www.dese.gov.au/collections/translations-belonging-being-and-becoming-early-years-learning-framework-australia>

Huduma ya Mkalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhalni wasiliana na shule ya mapema au huduma ya utotoni ya mtoto wako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia katika swali yako tafadhalni pigia simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na uombe mkalimani katika lugha yako. Opereta atapiga nambari ya simu unayotoa na kupata mkalimani kwenye laini kukusaidia na maswali yako. Hautatozwa kwa huduma hii.

Kujifunza shulenii

Kujifunza kwa mapema

Kuwa msemaji mzuri inamaanisha:

Watoto wanajua wanaweza kutumia nambari, kuhesabu na kupima katika maisha ya kila siku

Watoto wanaweza kusikiliza, kuelewa na kuunda hadithi na nyimbo

Watoto hushiriki hadithi kutoka kwa tamaduni zao na katika lugha zao

Watoto wanaweza kuwasiliana na kushiriki yale waliyojifunza kuitia muziki, uigizaji, sanaa na densi

Wanafunzi wanaweza kukuza na kutoa maoni yao wenyewe (Masomo: Kiingereza na Hisabati)

Wanafunzi wanaweza kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika ili kuwasiliana (Masomo: Kiingereza na Hisabati)

Wanafunzi wanaweza kutumia ustadi wa hesabu katika maisha yao ya kila siku (Somo: Hisabati)

Wanafunzi wanaweza kutumia teknolojia shulenii na katika maisha yao ya kila siku kuwasiliana na wengine (Somo: Teknolojia ya habari na mawasiliano)